KIZIDUO

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAMU KILICHOFANYIKA TAREHE 20.01.2022 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

A: WATAALAM WALIOHUDHURIA

1. Wakili Agape P. Fue - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) - Mwenyekiti
2. Ndg. Mikidadi B. Nasoro - Kaimu Afisa Utumishi (W) - Katibu
3. Ndg. Salima Kadinde - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
4. Ndg. Elias M. Jamvia - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
5. Mwl. Kennedy C. Bukagile - Afisa Elimu Msingi (W)
6. Ndg. Felis B. Mhando - Mtunza Hazina (W)
7. Ndg. Fredrick J. Kibwana - Mkaguzi wa Ndani (W)
8. Ndg. Damas Lubuva - Afisa Kilimo na Ushirika (W)
9. Ndg. Robert J. Sungura - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
10. Dk. Boazi P. Mnenegwa - Kaimu Mganga Mkuu (W)
11. Ndg. Secelela Dagaa - Afisa Ustawi wa Jamii (W)
12. Ndg. Pamella M. Kenyunko - Kaimu Afisa Biashara (W)
13. Ndg. Hamisi Hassan - Kaimu Afisa Nyuki (W)
14. Ndg. Ndimmyake Mwakapiso - Afisa Habari (W)
15. Ndg. Bilal Ramadhani - Kaimu Afisa Mazingira (W)
16. Ndg. Imani Mwakyoma - Kaimu Afisa Mipango (W)
17. Ndg. Felix A. Tossi – Kaimu Afisa Uchaguzi (W)
18. Ndg. Hillary Haule - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
19. Eng. Alex M. Foya - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
20. Ndg. Daniel Sichone - Kaimu Afisa Ugavi (W)
21. Ndg. Leonia L. Nduye - Kaimu Katibu TSC (W)

B: SEKRETARIETI

1. Ndg. Lukelo Mlawa - Katibu wa Kamati
2. Ndg. Gabriel Shayo - Katibu wa Kamati

**KMW/MUF/113/01/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao. Alisisitiza ushirikiano na michango ya mawazo muda wote ili kuleta ufanisi wa kikao kwa manufaa ya wananchi wa Mufindi na Taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 03:00 Asubuhi.

**KMW/MUF/114/01/2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda zifuatazo kuwa za kikao cha tarehe 20.01.2022

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Watalaam wa tarehe 21/12/2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Watalaam wa tarehe 21/12/2021
5. Kusoma na kusahihisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 23/12/2021
6. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango wa tarehe 23/12/2021
7. Kusoma na kusahihisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi, Ujenzi na Mazingira wa tarehe 13.10.2021.
8. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha Kamati ya Huduma za Uchumi Ujenzi na Mazingira wa tarehe 13.10.2021.
9. Kusoma na kusahihisha Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii wa tarehe 11.10.2021.
10. Yatokanayo na Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii wa tarehe 11.10.2021.
11. Kusoma na kusahihisha Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Kudhibiti UKIMWI wa tarehe 08.10.2021.
12. Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa Kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021.
13. Taarifa ya Fedha, Mapato na Matumizi kuishia 31 Desemba, 2021.
14. Taarifa ya utekelezaji ya miradi ya maendeleo Kwa Kipindi cha Oktoba - Desemba, 2021.
15. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za kitengo cha manunuzi kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021.
16. Taarifa ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021.
17. Taarifa ya mapitio ya mpango wa manunuzi wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
18. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za kitengo cha Sheria kwa kipindi cha Oktoba - Desemba, 2021

19. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021.
20. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za kitengo cha TEHAMA kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021.
21. Taarifa ya utekelezaji kazi za Idara na Vitengo; -
    - Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika.
    - Idara ya Mifugo na Uvuvi
    - Idara ya Ujenzi
    - Idara ya Ardhi na Maliasili
    - Idara ya Mazingira
    - Kitengo cha Nyuki
    - Idara ya Elimu Msingi
    - Idara ya Elimu Sekondari
    - Idara ya Afya
    - Idara ya Maendeleo ya Jamii
22. Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kamati ya kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha Oktoba – Desemba, 2021
23. Kufunga kikao

**KMW/MUF/126/01/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA OKTOBA - DESEMBA, 2021.**
Ilielezwa kuwa, Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri iliidhinishiwa kiasi cha Tshs **16,503,078,741.90** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo.

**MAPOKEZI YA FEDHA**
Ilielezwa kuwa, Kwa kipindi cha Julai, 2021 hadi Desemba 2021 Halmashauri imepokea jumla ya Tshs **5,316,117,159.10** sawa na asilimia **32.21** ya makisio ya mwaka.

**MATUMIZI YA FEDHA**
Aidha, Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021 Halmashauri imetumia jumla ya Tshs **3,006,532,664.71** ya fedha zilizopokelewa sawa na asilimia **56.56**. Kati ya fedha hizo Tshs **2,150,000,000** zilitumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 57 kwa shule za sekondari, vyumba vya madarasa 42 kwa vituo shikizi, bweni moja na nyumba ya mtumishi 3 in 1 kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO-19. Mchanganuo wa matumizi uliambatishwa kwenye taarifa. Changamoto na utatuzi wa changamoto hizo uliambatishwa kwenye taarifa.

**Majadiliano**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo, katika kujadili walizungumzia suala la kutolewa kiwango sawa cha fedha kwa utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa fedha za mapambano dhidi ya UVIKO-19 kutokana na utofauti mkubwa wa jiografia ya Wilaya ya Mufindi kwani umbali na upatikanaji wa malighafi za ujenzi ni mgumu kwa baadhi ya maeneo hivyo kufanya miradi kutekelezwa kwa ugumu. Pia walishauri

kuwa taarifa ziwasilishwe kwa mamlaka husika ili kwa baadae fedha ziletwe kulingana na uhalisia wa gharama za utekelezaji wa miradi kwa maeneo husika, aidha walisisitiza kutumia mfumo wa usimamizi uliotumika kwenye miradi ya UVIKO-19 kutumika kwenye miradi yote ya Halmashauri kwa kuwa umeonesha ufanisi mkubwa na miradi kukamilika kwa wakati. Taarifa ilipitishwa

**KMW/MUF/135/01/2022: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao kwenye kikao. Alisisitiza kuendelea na ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Halmashauri ili kuboresha utoaji huduma kwa jamii na kuhakikisha tunaleta maendeleo mazuri katika Halmashauri ya Wilaya Mufindi na Taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 08:50 mchana.

| | |
|---|---|
| ……………………………… | ……………………………… |
| KATIBU | MWENYEKITI |
| TAREHE 9/6/2022 | TAREHE 09/06/2022 |